

Kanuni za Ushirikiano

Makubaliano

Kanuni hizi zilikubaliwa na mukusanyo ya mashirika zihusikazo na kazi ya kiutu Kwa tarehe 12 Julai 2007

Mukusanyo ya mashirika zihusikazo na kazi ya kiutu, baada ya kuundwa kwake, Julai 2006, hukutanisha mashirika ya kimataifa na mashirika ya kibinadamu yasiyo ya kimataifa bila kuyatafautisha

- Kutumikika kwa ajili ya kuongeza nguvu ya kukamilisha kazi za kiutu zenye kutegema haki na jukumu ya kuhudumia wakahaji menye hitaji.
- Kutambua umbalimbali wa mashirika za kiutu kama vile jambo la muhimu katika kazi za kiutu, na kutambua kama ushirikiano kati ya mashirika haya ni jambo la muhimu.
- Kwa nia ya kujenga na kuimarisha ushirikiano mwema.

Mashirika ya kiutu katika mukusanyo ya mashirika zihusikazo na kazi ya kiutu yanakukubali kujenga ushirikiano wao juu ya msingi wa kanuni zifuatazo:

1. Usawa

Usawa analazimisha kuheshimiana kati ya mashirika yote bila kujali ukubwa au nguvu za kila shirika. Washiriki, lazima waheshimu mandeti (muda) jukumu na uhuru wa kila mmoja. Heshima kati ya mashirika siyo kizuwizi kwa mashirika ya kiutu kwa kutoa oni mbalimbali.

2. Uwazi

Uwazi unaonekana kupitia njia za mazungumzo (chini ya msingi wa usawa), mukazo ukitiliwa juu ya kushauriana na kubadilishana habari kwa wakati wenye kustahili. Mawasiliano na uwazi, pamoja na uwazi katika matumizi ya pesa, unaongeza kiwango cha kuaminiana kati ya mashirika za kiutu.

3. Mbinu za kutumika kwa ajili ya kuleta matokeo kamili

Kazi nzuri za kiutu zinapashwa kufanyika chini ya msingi waukweli na kuleta matokeo kamili. Kusudi ya kufikia shabaa hili, inahitajika kuwe uongozi wa pamoja wenye kuleta matokeo kamili.

4. Jukumu

Mashirika ya kiutu inakuwa na wajibu kila mumoja zidi ya mwingine, wakati wanapofanya kazi zao kwa bidii, kwa uadilifu na kwa namna yenye manufaa na kwa ginsi inayofaa. Ni lazima mashirika haya yawe na uhakika kwamba wakati yanapojitolea kufanya kazi fulani, yakuwa na rasilimali, na ujuzi, na uzoefu na uwezo wenye kustahili wenye kuwawezesha kutimiza ahadi zao. Kuepukana kwa zati na kwa nguvu zaukiukwaji wa sheria yanayotendwa na mashirika ya kiutu ni lazima pia kushurulikiwe daima.

5. Uongezeanaji

Umbalimbali wa mashirika ya kiutu ni jambo la muhimu tunapokua tukijenga juu ya mambo ya faida yetu tunaipata wakati tunapo pima uzuri wa kazi zetu na zile za wengine na kupitia michango ya kila mmojawetu. Uwezo wa mahali ni wa muhimu sana na wenye kustahili kuongezwa, na kutumiwa kama vile msingi wa kazi zetu.

Mashirika za kiutu zinapaswa kufanya nguvu ya kuingiza uongezeanaji ndani ya kazi yao.

Matatizo ya kilugha na vikwazo vya kitamaduni lazima vipate suluhisho.